**102/3 FASIHI**

**MUONGOZO WA KUSAHIHISHA**
**SEHEMU YA A(LAZIMA )**

1. a) Vitambulisho vya mtambaji bora.
   i. sauti nzuri inayosikika
   ii. Kumbukumbu nzuri
   iii. Matumizi ya toni
   iv. Matumizi ya viziada Lugha/ishara
   v. Matumizi ya miondoko/kunengua viungo vya mwili
   vi. Ushirikishi wa hadhira
   vii. Utambuzi na weledi wa hadhira
   viii. Uwezo wa ufaraguzi- kufanyia hadithi mabadiliko
   ix. Awe mcheshi/aibue kicheko kwa hadhira
   x. Uwezo wa kukadiria kasi wakati wa utambaji
   xi. Avae maleba
   xii. Makamavu
   xiii. Kuibua hisia zahadhira
   xiv. Aelewe lugha ya hadhira zozote (4x1 = 4)

b) Njia za kuihushisha hadhira.
i) Maswali
ii) Kushiriki unyimbo wanazoelewa
ii) Kuwapigishamakofi (2x2 =4
c) Mbinu anazotumia mlumbi ili kufanikisha uwasilishaji wa ulumbi
i) matumizi ya miondoko
ii) Matumizi ya mada zinazoafikiana na utamaduni wa hadhira
iii) Kuipaza sauti yake asike vyema
iv) Kuihushisha hadhira katika ulumbi
v) Matumizi ya alama ka fimbo .
vi) Uvaaji wa malema
vii) Ufahamu wa visa vya kihistoria vya jamii husika
vii) Ujuzi wa kutumia masolugha/ishara
ix) Matumizi ya lugha fasaha katika ulumbi
x) Kuwa na ukakamavu.
xi) Matumizi ya vichekesho
xii) Kuigiza ili kuibua hisia
xiii)Matumizi ya vipera vingine vya fasihi simulizi kama vile methali, ngano, nyimbo n.k
zozote 12x1 =12

**SEHEMU YA B TAMTHILIA YA KIGOGO**

2.“Wamenimaliza… wamenigeuka.”
**Weka dondoo hilI katika muktadha wake. (alama 4x1)**
i) Maneno ya mama pima yaani Asiya
ii) Anamwambia Tunu
iii) Wako katika soko chapakazi

iv) Hii ni baada ya kupinduliwa kwa seirkali ya majoka ambaye mamapima alikuwa mfuasi wake.

**B) Eleza namna msemaji amemalizwa na kugeukwa?(alama 4)**

i) Mambo yameanza kumuendeda segemnege (Kinyume)
ii) Serikari iliyopinduliwa ilikuwa inamwinda ili imuue.
iii) Anasema wamegeuka hata kufika kuimwaga pombe yake.
iv) Anaomba ulinzi kutoka kwa akina wanasogamoyo na tunu anamhakikishia usalamu.

**c) Eleza jinsi wahusika wengine walivyo maliziwa katika tamthilia. (alama 8)**

Tunu

Mwanaharakati huyu na kuvujwa mguu, Mpango wa awali ulikuwa ni kumuua. Hat hivyo alipona kwa bahati tu.

**Ngurumo**

Nngurumo ananyogwa na chatu hata baada ya kuwa na manufaaa makubwa katika utekelezaji maasi katika uongozi wa majoka.

Kijana huyu anajitolea kufanya kila anloambiwa na utawala lakini anaangamizwa kwa sababu alijua siri nyingi za uongozi .

**Chopi**

Ni mlinzi wa majoka ambaye anatekeleza maovu ya utawalakama vile mateso kwa kenga ipasavyo. Hivyo katika mwendelezo uo huo majoka na kenga wakubaliana kumuua Chopi ili asitoe siri zao.

**Jabali**

Alikuwa mpinzani wa karibu sana wa majoka. Alifanyiwa njama akauwawa kwa vile kilichoonekana kama ajali ya barabarani.

**<u>SEHEMU YA C. TAMTHILIA KIGOGO</u>**

3. Utawala wa majoka katika jimbo la sagamoyo umejaa sumu ya nyoka. ‘Jadili usemi huu kwa hoja kumi.

1. Unyakuzi wa ardhi. Majoka na mshauri wake wajitwalia eneo la soko la chapakazi ili wajenge hoteli ya kitalii jambo hili linasababisha madhara makubwa kwa wananchi waliokuwa wakitegemea soko hii kukimu familia zao.
2. Mauaji ya watu : vijana watano wanauwawa wakati wa maandamano na wengine wanaumia.
3. Kuna vitisho. Wanaharakati wanaopinga utawala wa majoka wanatishwa, kuna vikaratasi vinavyo rushwa katika makazi yao ili wahame.
4. Kuangamiza wapinzani wake; Jabali aliuwawa kwa njama za Majoka na chama chake kikasambaratika . Tunu kiongozi wa wanaharakati wa kudai haki nusura auawe. Yule aliyetumwa kutekeleza mauaji yake hakutimiza lengo lake.
5. Ukosefu wa utu. Majoka hadhamini utu/uhai wa mtu. Majoka anaamlisha watu wapigwe risasi bila kujali kuwa wana haki ya kuchagua viongozi wanaotaka.
6. Tengatawala: katika jimbo la Sagamoyo kuna sumu ya nyoka: yaani uhasama unapendwa na viongozi ili kuwagawa wananchi kwa mfano Sudi ana uhasama na Boza ambaye ni mchonga vinyango mwenzake . Sababu ya uhasama wao ni kwa kuwako katika milengo tofauti ya kisiasa. Aidha , Ngurumo na kundi lake la walevi tayari wameshatiwa sumu na utawala wa majoka, hivyo wanahasimu wanaharakati, Tunu na sudi.
7. Kuzorota kwa maendeleo. Jimbo la sagamoyo limetimiza miaka sitini ya uhuru lakini bado liko nyuma kimaendeleo.
8. Rushwa: Mamapima anatoa hongo ya uronda kwa Ngurumo ili apate mladi wa kukata keki ya Uhuru. Vilevile Boza na kombe wanapokea kipande cha keki kutoka kwa Kenga ili wawe wafuasi wa utawala wa majoka vivyo hivyo kwa ngurumo , ukataji wa miti.

a) utakaji wa miti

10. kufunga soko
11. Kubomoa viosiki
12. Kuongeza kodi

13. Kutoa kibali cha kuuza pombe haramu
14. Mapendeleo Mama pima anapewa mradi wa kuoka keki.
15. Uzalishaji wa dawa za kulevya
16. Ukwame wa majoka kwa kunyemelea Ashwa.
17. Anasa ya Husda kwa kujipondoa
18. Kutozingatia usafi wa soko/maziangira
19. Ukabila: Siti na kombe wanapata vijikaratasi wahame Sagamoyo.
20. Kudorora kwa kiwango cha ellimu ; Wanafunzi wa majoka academy wamekuwa makabeji.
21. Matumizi ya vyombo vya usalama /askari/polisi kuzima maandamano
23. Kudhibiti vyombo dola na kuweka watu kwa seli bila hatia.
24. Matumizi mabaya ya raslimali/mikopo. (20x1=20)

. **SEHEMU YA C USHAIRI A.**
4. a) Ukawafi – Mishororo ya kwanza mitatu ina vipande vitatu
Msuko- Kibwagigo ni kifupi
Tarbia – Mishororo minne kila ubeti
Ukaraguni – Vina vinavyoftofautiana
Kikwamba kianzio nyoosha mkono

b) Msimamo dhabiti katika utetezi wa haki, kataa kudhulimiwa na uungane na wenzako, lazima uwe na usajiri. 2x2 =4

c) Inuka kwa ujasiri kama ishara ya kutoridhika kwa sababu unadai haki yako kwa njia halali.
- Simama imara na ukatae kudhulumiwa na utashinda. 4x1 alama 4
d) Taswira – nyooosha mkono
-Misemo - Kula njama-
- Uhuishi/ tashihisi – Sauti inayojaa kitisho. Inksari jiunge – ujiunge
e) Lahaja – Mangi,- Kuboronga- yaondoke masumbuko, masumboko yaondoke
f) Toni ya – kutoridhika/kulalamika kuhamasisha/kuzindua. (alama 2)
g) i) Mateso, taabu
ii) JIkaze/ Jikakamue/Jitolee/Kujibiidisha. 2x1= alama 2

**AU**
5. a) Kuonyesha madhila anayopitia mwanamke/mama mikononi mwa mwanaume.
b) Ngonjera – ni mazungumzo kati ya Mama na Mwana. (1x2 = alama 2)
c) Kufanywa kufua nguo (aina 1, idhibati 1; jumula alama 2)
Mama huenda shambani peke yake.
Baba hubaki nyumbani tu na kupiga ngumzo mitaani
Baba hamthamini mama
Mama hukata kuni kondeni na kuzibeba kichwani.
Mama akichelewa kufika nyumbani akitoka kondeni huadhibiwa.
Mama ndiye hutafuta chakula( yoyote 5x1 =5)

d) Ubeti una mishororosita.
Mishororo imegawika katika vipande viwili isipokuwa mshororo wa tano ambao umegawika katika kipande kimoja.
Kila mshororo una mizani kumi nasita isipokuwa mshororo wa sita ambao una mizani tano.
Kibwagizo kimefupishwa/ mshororo wa mwisho umesukwa.
Mjpangilio wa vina
bu , ni
bu, ni

bu,ni
bu,ni
e
mbe,go (alama 1 kwa kila jibu sahihi, jumla alama 5)

e) Umenifanya nihisi uchungu ambao nimekuwa nao kwa miaka mingi , usidhni kuwa nayapenda madhira na mashaka, nakerwa na hali yake ya kunidhibiti kufanya jambo na sasa nimechoka, ninaanza kwa hakika kujitayarisha kwa mapambano, hilo nakwambia. (alama 4)
f) Jaza – Malipo kwa kutenda wema/shukrani/asante (alama 1)
ii) Muhibu – Mpenzi (alama 1)

**SEHEMU YA D. HADITHI FUPI TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE**

6. a) Jadili matatizo yanayowakumba wakazi wa mandogoporomoka katika Tumbo Lisiloshiba. (alama 10)

i. Wanamadongoporomoka wanadharauliwa na kutwaliwa ardhi yao.
ii. Kuporwa aridhi yao imenyanyaswa na tabaka la mabwanyenye.
iii. Wanawatoa katika ardhi yao na kuvunja vibanda vyao pasipo hata kuwalipa fidia.
iv. Unyanyasaji huu unafanywa kwa wakazi hawa kwa kuwa hawana mtetezi.
v. Haki imenunuliwa na wenye nacho. Wanabomolewa vibanda vyao ilhali hawajaonyeshwa mahali mbadala pa kweda kuishi.
vi. Ukosefu wa haki: Watu wa mandogoporomoka hawana haki wenye fedha wanawaona wakazi hawa kama takataka tu.
vii. Ardhi ya madongoporomoka inaponyakuliwa na wenye nacho wanashindwa kupata mtetezi . wanasheria wamenunuliwa na matajiri ni vigumu kupata mwanasheria mwaminifu. Mzee Mago anashauriana na wenzake namna ya kurukaviunzi hivi vya kisheira.
viii. Makazi duni : Wakazi wamadongoporomoka wanaishi katika makazi yenye mandhari chafu. Kulikuwa na mashonde ya vinyesi.
ix. Wanaishi katika vibandachwara vinavyozungukwa na uozona bubujiko la maji machafu. Hakuna mamlaka yoyote ya maji taka inayojishughulisha nao.
x. Wakazi madogoporomoka wananyimwa fidia inayolingana na thamakni ya makazi yao yaliyopokonywa na mambwanyenye.
xi. Watu wa madongoporomoka wanaachwa njaa baada ya jitu kubwa kula chakula chote . Jitu linaingia katika mkahawa mshenzi na kuagiza kila chakula kilichopo kiletwe . jibu linabugia chote huku watu waliokuwa wamesubiri chakula hicho wakibakia njaa.
xii. Wakazi wa madongoporomoka wanabaguliwa sehemu wanaoishi hakuna maendeleo yoyote kuna uchafu mwingi sana sehemu hii ilipaswa kusafishwa ili walau ifafanane na sehemu nyingine za mji ho.
xiii. Wanamadongoporomoka wamekosa usalama. Wanaishi kwa wasiwasi sana. Wanaamshwa kwa vishindo vya mabuldoza .
xiv. Askari wa baraza la mji wanaangusha vibanda vyao na kuwatimua waliokuwa bado wamelala. Jeshi la polisi linawapa ulizi askari kwa mirau na bunduki Mali zao duni zinaharibiwa.
xv. Wanadongoporomoka wanalia na kulalamika kwa kukandamizwa na vyombo vya ulinzi. Wanakandamizwa kwa sababu ya umaskini wao . Matajiri wanawakandamiza. (10x1)

6. b) b) **Ubadhirifu wa mali ya umma umetamalaki katika hadithi ya Shibe Itatumaliza. Jadili kwa kutoa mifano mwafaka. (alama 10)**

Mzee Mambo analipwa msharahra mnono kama mkuu wa wizara zote ilhali kila wizara ina waziri wake.
i) Sherehe kubwa za viongozi wa serikali ziantumia mali ya umma. Hivyo basi kuchangia ubadhilifu wa mali katika jamii.
ii) Viongozi huendeleza ubadhirifu kwa kutumia mali ya umma kwa manufaa yao wenyewe. Magari ya serikari ykanatumika katika sherehe na kazi za nyumani kama vile kuleta maji katika sherehe.
ii) Vyakula katika sherehe vinanunuliwakwa jpesa za umma. Pesa hizi zingetumika kuendeleza asasi za kijamii.
iv) Ubadhirifu unadhihirishwa na DJ jpale anapokea mabilioni ya pesa kwa kuwatumbuiza wageni katika sherehe.
v) Ubadhirifu unadhihirishwa na viongozi wa serikali wanaowachukua watu wao wa karibu na kuonelea wamefaidika kutokana na rasilmali za wanajamii bila kuzitolea jasho.
vi) Viongozi wa serikali kama vile Sasa na Mburawanaamua kujipakulia chakula kupita kiasi katika shereh za mzee mambo na jamii yake ubadhirifu wa mali ya umma unaonekaran ambapo mali ya umma inatumika kuwaajiri mawaziri wawili wenye majukumu sawa katika wizara moja kazini . Kazi hii ingefanyw ana waziri mmoja na mshahara wa waziri wa pili ungechangia katika kuinua sekta nyingine.
vii) Upeperushaji wa matangazoa ya sherehe ya kiongozi binafsi katika vyombo vya haari kitaifa kwa siku nzima ni ubadhirifu wa mali ya umma. Pesa zilizotumika zinagechangia pakubwa katika kuinua uchumi wa taifa.
viii) Uuzaji wa dawa zilizotolewa katika bohari la kitaifa katika duka la DJ ambayo ni biashara ya mtu binafsi ni ubadhirifu wa mali ya umma.
ix) DJ kulipwa kutumbuiza watu katika sherehe ya Mzee Mambo na kulipwa mabilioni ya fedha ni ubadhirifu wa mali ya umma.
x) DJ kupewa kazi ya mipango na mipangilio katika sherehe ilhali kuna mawaziri wawili wanaolipwa mshahara kwa kazi hiyo ni ubadhirifu wa mali ya umma. (zozote 10x1 =10)

**7. a) Majibu**

a) Maelezo ya mwandishi /Msimulizi kuhusu Otii pale nyumbani Kitandani Otii alirejelea maisha yake ya awali, aliumia muguu na kupoteza umaarufu wake.
Otii alikuwa amerejeshwa pale nyumbani mwke kwa amri ya daktari angojee kifo.
Otii alipovunjika mguu na kutumia mikongojo miezi sita, alikataa kurejelea kandanda uwanjani.(4x1=4)

b) Otii alikuwa uwanjani akichezea timu ya bandari FC.

- Kutokana na uhodri wake alikuwa mwiba kwenye timu kinzani ya Yanga kwene kinyang'anyirocha kuwania kombe la klabu bingwa Afrika mashariki na kati.
- Alikuwa amewala chenga mabeki wote wa Yanga na kuelekea kufumua kiki kali kwenye eneo hatari , ndiop jibabajoja la miraba minne lilipomkwaa akaanguka
- Alianguka vibaya kama gunia la chumvi. Picha ya eksirei ilionyesha kuwa amevunjika mfuka wa muundi na nguyoni.
- Baada ya kuumia aliterekezwa kabisa na maafisa wa Bandari FC
- Hata maafisa wa serikalini hawakumjali hata kidogo
- Alitupwa kama masimbi na hakuna aliyemkumbuka
- Maumizu na mates hayo ndiyo kuumwa na nyoka.

c) i) Ukosefu wa utu

- Mwandishi anonyesha kuwa utu umepotea na haupo tena katika jamii.
- Otii anatoa mchango mkubwa kwa kuichezea timu ya Bandari FC na hatatimu ya taifa ya Harambee lakini anapovunjika mguu hakuna anaejali kipaji chake.
- Hakuan fidia anayopewa hata baada ya kuacha mchezo huo kwa kuumizwa.\
- Chama cha waqtu wa nyumbani wananza kujadili mazishi ya mtu akiwa bado hai.
- Wanachama wa chama cha nyumbani wanakosa utu na kuanza kujadili kusafirisha maiti ya Otii wakati Otii bado yu hai an anawasikiliza.

- Rehema anakosa utu kwa kumwambukiza Otii Maradhi.

ii) Umuhimu wa kuzingatia ushauri

- Otii anaitwa na rafiki yake na kushauriwa dhidi ya kujihushisha na msichana mrembo Rehema Wanjiru.
- Otii anapuuza ushauri huo na kusema kuwa yuko radhi kuwa nzi na kufia kidondani.
- Matokeo ni kuwa rehema anamuambukiza ugojwa wenye dalili za Ukimwi.Wotw wawili wanafariki mtawalia.
- Otii anamshauri mwenyekitiwa chama nyumbani azikwe Mombasa.Wao walikataa ushauri huo.
- Baaaday wanajkpata ajali mbaya.

8. “Dada Umu, Di, ni mimi, Ni mimi ndugu yenu . Ni hai Auntie Sauna aishikwa na polisi”.

Weka dondoohilikatikamuktadha wake. (alama4)
Jibu
Maneno haya yalisemwa na Mwaliko.Alikuwa akiwaambia Umulkheri naDick . Tendio hili lilitukia katika mkahawa na Mjaliwa walipokutana kisadfa. Hii ni baada ya mwaliko kumepeleka babakemlezi maeneo yale kusheherekea siku ya kuzaliwa kwake.

**Fafanua sifa tatu za msemaji (alama 6)**
**Jibu**
Msemaji ni mwaliko . Ana sifa zifuatazo.
Mwenye maadili mema, Mwaliko alipolelewa mwangemi na Neema aliinuka kuwa ghulamu ya hali ya juu akiwaheshimu wazazi na majirani na kuwatii wazazi.

Mwenye shukrani- Mwaliko aliamua kumnunulia babake chakula cha mchana siku yake ya kuzaliwa kwenye hoteli ya Majaliwa .

Mwenye bidii- Alifanya bidii masomoni hadi kufikia chuo kikuu . Alisajili kwa shahada ya uzamili katika taaluma ya mawasiliano na kuhitimu . Mwaliko anafanya kazi yake kwa bidii ya mchwa.
Zozote =3 (3x2 =6)

**Taja tamathali moja ya lugha iliyotumika katika dondoo (alama2)**

**Jibu Kuchangaya ndimi –Auntie**

**Ni kwa nini Aunitie Sauna alishikwa na polisi? Eleza kikamilifu (alama 8)**
**Jibu.**
Baada ya Umu kupiga ripoti kwenye kituo cha polisi kuwa nduguze wanuna wamepotea, polisi walifanya uchunguzia wao na kujua kuwa walitekwa nyara. Aliyetekelea kitendo hiki ni kijakazi Sauna . Sauna alikuwa akimfanyia biashara Bi Kangara. Polisi walipojua mahali alikokuwa akijificha Bi Kangara, walishika jia hadi nyumbani kwake ambako waliwatia mbaroni. Bi Kangara na Sauna Walifikishwa mahakamani na kushtakiwa kwa kosa la ukiukaji wa haki za watoto hivyo basi wakafungwa miaka saba gerezani na kazi ngumu.